

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA
MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE
ALIYOITOA KWENYE KILELE CHA
MAADHIMISHO YA WIKI YA NENDA KWA
USALAMA BARABARANI MKOANI RUKWA
KATIKA VIWANJA VYA NELSON MANDELA
TAREHE 12 NOVEMBA, 2016**

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani
Mkoa wa Rukwa,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
Katibu Tawala wa Mkoa,
Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rukwa,
Wajumbe wa Kamati ya Usalama Barabarani
Mkoa wa Rukwa,
Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi,
Wageni waalikwa,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana.

- Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kukutana mahali hapa siku ya leo tukiwa na Nguvu na wenyewe Afya ya kutosha katika maadhimisho haya muhimu ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Ndani ya Mkoa wetu wa Rukwa.
- Kwa namna ya pekee ninapenda kuwashukuru waandaaji wa shughuli hii ya leo kwa heshima kubwa mliyonipa ya kuwa Mgeni rasmi,
“Asanteni sana”
- Kipekee nichukue fursa hii kuwapongeza watumiaji wote wa Barabara na vyombo mbalimbali vyatengeneza na hata wale ambao ni watembea kwa miguu kwa kushiriki katika maadhimisho haya. Natambua kwamba kwa muda mrefu utaratibu huu wa kuwa na wiki moja ya kujikumbusha mambo ya msingi

kuhusu usalama wetu tukiwa Barabarani na vyombo vyetu umekuwa ukifanyika. Jambo kubwa ikiwa ni elimu ili kuepukana na ajali zisizokuwa za lazima kukatisha maisha ya watu na kuharibu vyombo vichache vya usafiri tulivyo navyo. Maadhimisho haya yanatoa uhakika kwamba kila mtu ana haki ya kutumia barabara kwa utaratibu unaozingatia Sheria na Kanuni.

Ndugu Mwenyekiti,

- Naamini hakuna mtu hata mmoja kati yetu anayependa kupata ajali, majeraha ama kupoteza maisha. Hata hivyo naamini kwamba kila mmoja wetu amewahi kuguswa na ama kufikwa na majanga ya ajali kwa kujeruhiwa ama kupoteza ndugu, jamaa, rafiki ama jirani yake. Tunapotumia Barabara na vyombo vyetu vya usafiri tunafurahia lakini ni muhimu sana

kuweka nafasi kubwa ya kutunza usalama wetu wakati wote. Ili tuishi tusipatwe na ajali tufanye nini:-

- (1) Tutekeleze, kuziheshimu na kufuata Kanuni za Barabarani ikiwa ni pamoja na alama za kuongoza, kuonya, kuamuru, kukataza, kuruhusu na Taarifa.
- (2) Tuhakikishe tunazingatia sheria zilizopitishwa na Bunge kwa ajili ya kumlinda kila mtumiaji wa barabara na vyombo vyetu vya usafiri.
- (3) Tuhakikishe kwamba vitendo vyetu vyote vya kibinadamu ambavyo vinachangia kusababisha ajali tunaviepuka; hii ni pamoja na:-
 - (i) Mwendo kasi,
 - (ii) Ulevi,
 - (iii) Kuzidisha uzito na ama abiria,
 - (iv) Kuegesha ovyo barabarani,

- (v) Kupita gari la mbele sehemu ambayo haistahili kama kwenye kona, mlima, daraja, mteremko mkali n.k.
- (vi) Kuegesha gari barabarani usiku bila ishara ya kung'ara,
- (vii) Kupuuza vivuko vyta watembea kwa miguu,
- (viii) Kupuuza kuvalaa kofia ngumu kwa waendesha na wapanda pikipiki,
- (ix) Kuacha mifugo kutangatanga ovyo barabarani bila mwangalizi,
- (x) Kupakizana mshikaki kwenye pikipiki,
- (xi) Vyombo vibovu barabarani,
- (xii) Matumizi mabaya ya taa usiku,
- (xiii) Kuendesha bila kujali mazingira ya barabara, wingi wa watu na shughuli, hali ya hewa na uwezo wa kuona.

(xiv) Kuwaacha watoto wadogo kwenda au kucheza barabarani.

- Mambo haya na mengine ambayo sikuyataja Askari wa Usalama Barabarani namba moja ni Binadamu. Asilimia kubwa ya ajali zinazotokea zinachangiwa na sisi binadamu. Siku hizi kiasi cha fedha za adhabu zinazotokana na taarifa za usalama Barabarani kila mara utakuta ni nyngi na wanaotozwa faini hizo ni watu kwa kwenda kinyume na ama kupuuza sheria za usalama Barabarani.

Ndugu Mwenyekiti,

- Nimeambiwa kwamba Ajali zimepungua kwa Asilimia 18.3 Mwaka huu ukilinganisha na Mwaka jana. Ajali hizi bado ni nyngi sana kwa kuwa zimeweza kugharimu maisha ya watu wapatao 29 katika Mkoa wetu wa Rukwa.

Tusiridhike na matokeo hayo. Tuendelee kupambana. Hatutaki ajali; Tunataka kuishi.

- Natoa wito kwa Wananchi wa Rika zote katika Mkoa wa Rukwa tuone umuhimu wa kulinda maisha yetu tusipatwe na ajali za Barabarani bila mzaha na mbwembwe. Natoa wito pia kwa wadau wote wenyewe jambo la kuchangia kuepusha ajali za Barabarani wafanye hivyo kwa kushirikiana na Polisi kupitia Kikosi cha Usalama barabarani.
- Natoa wito kwa wananchi wote kutokubali ama kufumbia macho vitendo vya kuhatarisha maisha ya wengine badala yake watoe taarifa kwa vyombo vinavyohusika na hatua zinazostahili zichukuliwe mara moja.
- Nitoe wito kwa Kikosi chetu cha usalama Barabarani kuwa makini kwa kuhakikisha

utendaji wao unalenga kuelimisha na kuwalinda watumia barabara na vyombo vyao kwa usalama bila uonevu ama kukomoana. Mtu anayefuata sheria atambuliwe kwamba ni muungwana na hata anapofanya kosa dogo mara moja aelimishwe, aonywe na kutakiwa kurekebisha kosa dogo alilofanya.

Ndugu Mwenyekiti,

Miundombinu ya barabara ndani ya Mkoa wetu inaendelea kuboreshwa. Kitakwimu Mtandao wa Barabara ndani ya Mkoa wa Rukwa umefikia Kilometra 3,739.38. Katika mtandao huu:-

- (i) Barabara kuu ni Km 407.94 ambapo asilimia 88 ya barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha lami. Wakandarasi wanaendelea na kazi hasa katika barabara ya Sumbawanga – Chala – Kanazi, Kanazi – Kizi – Kibaoni na Matai – Kasanga Port.

(ii) Barabara za Halmashauri ni Km 2,528.78.

Ambapo Km 436.68 ni barabara za changarawe na Km 1,857.6 ni barabara za udongo. Zote hizi zinaboresha na zinapitika wakati wote.

- Hadi sasa yapo matumaini ya barabara ya Matai – Kasesya (Km 50) ambayo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Maandalizi ya kupata Mkandarasi yanaendelea.
- Barabara hizi zinapoboresha watumiaji wawe waangalifu kwa kuwa tunategemea baada ya barabara hizi kukamilika vyombo vya usafiri vitaongezeka.
- Halmashauri ziendelee kuboresha barabara za vijiji ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

- Tutunze barabara zetu pamoja na alama zinazowekwa.

Kwa moyo wa dhati kabisa tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada inazofanya kuleta Fedha za Miradi ya Barabara kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya barabara hizo zinakwenda Vijijini ili kuharakisha maendeleo yao. Hakika huku ndiko kukataa Ajali kwenyewe.

Ndugu Mwenyekiti,

- Tangu maadhimisho haya yalipofunguliwa Tarehe 5 Novemba, 2016 mmeefanya kazi kubwa ya kutoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri na watembea kwa miguu juu ya tahadhari wanazopaswa kuchukua wawapo

Barabarani katika maeneo mbalimbali hususan Mashulenii na Maeneo yenyeye mikusanyiko ya watu kama vile sokoni na maeneo mengine. Nawapongeza sana kwa zoezi hili kwa kuwa limeongeza kwa kiasi fulani uelewa wa Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa Barabara.

- Kwa umuhimu wake suala hili sio la kusubiri Wiki kama hii kila mwaka. Ni vema likawa endelevu kwa kuwa matumizi ya barabara ni jambo la kila siku ya maisha yetu.

Ndugu Mwenyekiti,

- Sote tunatambua kuwa Jeshi Ietu la Polisi hususan kitengo cha Usalama Barabarani ni kiungo muhimu katika kupambana na ajali za barabarani zinazotokea mara kwa mara. Nimeambiwa kwamba Kauli mbiu ya wiki ya

Nenda kwa usalama Barabarani kwa Mwaka huu ni "**HATUTAKI AJALI TUNATAKA KUISHI SALAMA**". Nitafarijika sana endapo nitaona kaulimbiu hii ikitekelezwa kwa Vitendo, uadilifu, uaminifu, uhodari, ushupavu, kujituma na kupinga uonevu na vitendo vyta kutoa ama kupokea Rushwa kwa pande zote katika suala hili. Nasisitiza saaaaaana washirikiane na vyombo vingine kama SUMATRA, TRA, TANROADS, BIMA HALMASHAURI NA sekta zingine hata zile ambazo sizo za kiserikali.

Nitoe wito Shirika la Bima la Taifa na Makampuni ya Bima itizame njia bora za kuwasaidia wahanga wa ajali hasa kuhusu fidia. Wanahangaika sana na kupata usumbufu mwingi bila msaada. Wanahitaji kusaidiwa kuongozwa. Wenye magari yaliyohusika na

ajali wakifuatwa wanawapiga chenga. Jambo jili linahitaji kukomeshwa.

- Mikakati ya kupambana na Matukio ya Ajali mliyoieleza katika Risala yenu ni mizuri. Simamieni na Tekelezeni kwa Vitendo mikakati hiyo mkiwashirikisha wadau mbalimbali hususan katika eneo la utoaji wa Elimu ya Usalama Barabarani kwa Wananchi. Vitumieni vyombo vya Habari tulivyonyavyo hususan Redio za ndani ya Mkoa wetu ambazo masafa yake yanafika hadi maeneo ya Vijijini. Naamini Wadau wote tukishirikiana kwa nguvu zetu zote tutaweza kupunguza idadi ya Ajali ndani ya Mkoa wetu.

Ndugu Mwenyekiti,

Natoa wito kwa wamiliki na madereva wa vyombo vyote vya moto wahakikishe

vinakaguliwa lakini pia amdereva wapime afya zao hususan macho ambayo ni sehemu muhimu katika kuendesha.

Mwisho napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru tena kwa kunialika na kwa maandalizi mazuri ya hafla hii ya leo. Nimeona watu wengi wamejitokeza kushiriki kwenye maandamano siku ile ya ufunguzi na leo tukiwa tunahitimisha wiki yetu ya Nenda kwa usalama Barabarani. Hii inaonesha ni kwa namna gani ambavyo tunahitaji kweli kuishi salama bila ya matukio ya Ajali za barabarani. Naamini Mwaka ujao tutakapokuwa katika maadhimisho kama haya tutakuwa tukijipongeza kwa kupunguza kwa kiasi kikubwa matukio ya Ajali za Barabarani na ama kwa kuyamaliza kabisa.

Niwapongeze Mwenyekiti na Kamati yake yote ya Usalama barabarani. Naamini wataendelea kutafuta mikakati bora zaidi ya kuepusha ajali na mikakati bora ya kuimarisha ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na Wananchi.

Natamka sasa kwamba maadhimisho haya yamehitimishwa kwa matarajio kwamba mafunzo ni endelevu.

***"HATUTAKI AJALI TUNATAKA KUISHI
SALAMA"***

Asanteni kwa kunisikiliza

Zelote Stephen Zelote
MKUU WA MKOA WA RUKWA